



GENIUS EXAM 2024



KCSE PREDICTION - 2024 -

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Saa: 2½

Jina: Nambari:

Mkondo: Sahihi:

Shule:

Maagizo

- (a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihamu katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (b) Andika mkondo wa Kidato chako kasha tia sahihi yako na uandike tarehe ya mtihamu katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (c) Jibu maswali yote
- (d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
- (e) Majibu yote sharti yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- (f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki
- (g) Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa. Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
- (h) Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

FOR MARKING SCHEME CALL/WHATSAPP 0790906300



GENIUS EXAM 2024



1. UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata

Mara moja akampigia mwanawe simu. Akamzoea na kumwambia atume ambulensi mara moja. Aliposita, mama akamwambia simu ya pili atakayopiga itakuwa ya polisi nay a tatu ya kituo chochote cha habari. Wakati huo Lilia yu pale, anayasikia lakini kwa mbali. Baada ya kupiga simu, namna mtu akajishughulikia kumtafutia mkazamwana mavazi ya kumkinga na baridi. Alipojaribu kumvisha, maumivu yakamzidia. Kabla ya kupoteza fahamu, Lilia aliusikia mlio wa ambulensi kwa mbali.

Alipozinduka, alijipata kitandani. Chumba cheupe pe! Yu peke yake. Lazima ni chumba cha wagonjwa wenye chao. Siku tatu akawa pale kitandani, hajiweza . hajiweza . Mama mkwe yuaja kila siku kumuuguza mkazamwana. Hakuona hata kivuli cha mumewe. Wale hakumuuliza mama mkwe alikuwa wapi mwanawe.

Siku ya nne, aliamka na kupata hakuwa peke yake. kuna mtu kando yake lakini asingeweza kumtambua maana kafungwa bandeji usoni. Mguu mmoja umeinuliwa, bila shaka ulikuwa umevunjika. Lazima ameletwa usiku wakati Lilia akiwa amelala fofofu, usingizi uliochochewa na dawa alizokuwa akipewa. Lilia hakumwangukia sana, maana dawa zilimlelea. Alilala tena.

Mchana alipokuja mama mkwe, akaelekea kwenye kitanda cha Yule mtu. Lilia hakuelewa , labda mama mtu alimjua mgonjwa Yule.

‘Bwana Gavana , uko hapa?’ mama akamuuliza mgonjwa. Lilia akashtuka. Gavana yupi huyu na mbona wamo chumba kimoja? Mgonjwa hakujibu, alighuna tu. Ikawa mama akija anakwenda na kumjulua hali mgonjwa huyo, kasha anarudi kwa Lilia kumshughulikia. Lilia alipotaka kuuliza alikuwa nani Yule, mama akamnyamazisha. Hakuwa na nguvu za kumshawishi mama kumwambia mengi. Akalala tena.

Siku tatu zikapita. Lilia amepata nafuu kidogo, hamjambo sasa. Mgonjwa mwenzake amepata watu wanaokuja kumtembelea. Wengi lakini hajaona mtu ambaye aonekana kuwa jamaa yake. Marafiki tu na wafanyakazi ambao walikuwa wamekunja nyuso zao. Jioni ya siku ya tatu akawasikia wauguzi wakisema mgonjwa huenda asiweze kutembea tena maana alihusika katika ajali mbaya sana. Nusura aage dunia lakini siku zikawa hazijatimia!.

Siku ya nne , mama mtu akaja. Akamwendea Yule mtu. Akamwangukia kwa muda. “Luka! Luka!Luka!” Lilia akamshangaa. Siku nne amekuwa chumba kimoja na mumewe na hana habari? Mama mtu akaendelea. “Yu wapi kirukanjia wako?” wajua yuko wapi? Amekuja siku ya kwanza kukuona . Siku ya pili alipoambiwa na daktari kuwa huenda usiwahi kutembea tena, aligeuka na kuondoka. Hajaonekana tena. Waona sasa? Uliacha mbachao kwa mswala



GENIUS EXAM 2024



upitao. Ulimfanya mkeo ngoma kwa sababu ya hawara ambaye hakuthamini hata chembe. Sasa angalia. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!”

Mama mtu alimgeukia mkazamwana na kumwambia kuwa daktari ashasema kuwa ameruhusiwa kwenda nyumbani. Lilia aligeuka na kumwangukia mumewe. Hakuwa na hakika, lakini alidhani aliona chozi moja likitiririka kutoka jicho lake la kushoto ambalo halikuwa limefungwa kwa bandeji.

Maswali

- a) Taja methali **moja** ambayo inaoana na kifungu hiki. (alama 2)

.....

- b) Kwa hoja **mbili** thibitisha kuwa Luka alimtelekeza mkewe. (alama 2)

.....

.....

.....

- c) Je, ni kweli mavyaa wa Lilia hakuwajibika? Toa sababu tano. (alama 5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- d) Taja mambo **mawili** yanayoonyesha kuwa watu hupewa huduma kulingana na nafasi zao katika jamii. (alama 2)

.....

.....



GENIUS EXAM 2024



.....

.....

e) Kulingana na kifungu, Lilia alilazwa hospitali kwa muda gani (alama 1)

.....

f) Eleza maana ya ; (alama 3)

i. Wenye chao.....

ii. Kirukanjia wako.....

iii. Fadhila za punda.....

2. UFUPISHO (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Suala la jamii kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na lishe ni jambo ambalo halina budi kushughulikiwa hjwa dhati. Chakula ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi binadamu na kila mja ana haki ya kupata chakula na si chakula tu bali chakula chenye vurutubisho muhimu. Nchi isiyowakimu raia wake kwa chakula ni sawa na ngombe aliyeshindwa kumnyonyesha ndama wake.

Kwa muda mrefu, viongozi wamekuwa wakipambana na tatizo la ukosefu wa chakula. Msimu wa kiangazi unapobisha hodi, watu wengi hasa wale wahitaji, hupukutika kutokana na mng'ato wa njaa. Japo serikali na wafadhili hutuma vyakula vya msaada kwa jamii zilizoathirika zaidi, chakula hiki huwa kama nguo ya kuazima, na bila shaka ya kuazimia haikidhi haja.

Mojawapo ya vyanzo vikuu vya uhaba wa chakula ni kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula chenyewe. Zipo sehemu nyingi nchini ambazo ni kame. Sehemu hizi hukabiliwa na ukosefu wa maji kwani, ama mvua hainyeshi, au inaponyesha haitoshelezi mahitaji ya mimea. Mimea mingi hujikaukia ikiwa michanga haina majina kudhihaki juhudi za wapanzi. Zipo sehemu katika nchi hii ambazo huenda kwa misimu hata zaidi ya mitano bila kupata zao lolote kutoka mashambani. Hali ikiwa hivi makali ya uhitaji huzidi na wakazi wa sehemu hizi hulazimika kwa wategemezi kwa majirani na serikali. Wengine wanapokosa chakula kabisa huazimia kula visivyoliwa. Wanaamwa la mbwa baada ya kukosa la mama.

Hali kadhalika, japo zipo sehemu nyingine ambazo hazina tatizo la ukame, mbinu hasi za kilimo husababisha utoaji wa mavuno haba, hivyo kutojitosheleza kwa chakula. Bila shaka wanapopanda ovyo, wanavuna ovyo, kuna wakulima ambao hupalilia mmonyo kwa udongo kwa kulima kandokando ya mito, kupanda zao lile lile katika sehemu ile ile ya ardhi miaka rudi, na

FOR MARKING SCHEME CALL/WHATSAPP 0790906300



GENIUS EXAM 2024




kutopanda mimea ambayo hukinga tabaka la juu la udongo dhidi ya kumomonyolewa na maji na upepo. Matokeo ya haya yanaweza kutabiriwa, udongo wenye rutuba huoshwa na mashamba kutwaa utasa ambao huzidisha kuzalishwa kwa chakula haba. Wakulima wengine hukaidi wito wa kupanda mimea ambayo hustahimili ukame kama vile mibaazi, mihogo, mtama, ulezi wa wimbi. Baadhi ya wafugaji hufuga mifugo wengi ambao hushindwa kustahimili kiangazi, si ajabu kupata kwamba katika baadhi ya maeneo mizoga ya ng'ombe na hata ngamia imezagaa kote, tanuri la kiangazi linapofanya kazi yake.

Sehemu nyingine zimebarikiwakwa ukwasi wa chakula. Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa sehemu hizi hawana mwao kuhusu umuhimu wa lishe bora. Wapo wanaodhani kuwa chakula ni chakula bora tumbo lipate haki. Hawa hula vyakula kama vile viazi, mahindi, na wengine nyama bila kujua wanahitaji vyakula vyenye virutubisho muhimu, yaani wanga, protini, vitamin na madini. Wapo wanaodhani kuwa protini pekee ni nyama. Hawa hula nyama kila wakati, matokeo yakiwa kuambulia magonjwa kama vile shinikizo la damu.

Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula, serikali kupitia wizara husika, imeanzisha miradi ya kuhakikisha kuwa kuna uzalishaji wa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Visima vya maji na mabwawa vimechimbwa katika sehemu kame ili kunyunyuzia mashamba. Baadhi ya wakulima wameanza kupanda mimea ambayo inapevuka na kutoa mazao haraka. Ipo mimea ya kuatika ambayo hutoa matunda baada ya muda mfupi, hivyo kusaidia kupunguza makala ya njaa. Wafugaji wengine wameanzisha miradi ya kufuga kuku wa kututumuliwa. Hawa hukua na kukomaa kwa muda mfupi na huweza kutoa nyama na mayai. Wafugaji wa kuku hawa huweza kuwauza na kununua aina nyingine ya vyakula.

Wakulima pia wanahimiza kutumia njia za kisasa za kuzalisha na kuhifadhi chakula. chakula kinapohifadhiwa vyema, hata mvua isiponyesha, raia huweza kujitegemea. Ikiwa maghala ya halmashauri za kuhifadhi chakula nchini hayahifadhi chakula. mara nyingi nchi hulazimika kuagiza chakula kutoka nje kiangazi kinapojiri. Aidha, Chakula kisipohifadhiwa vyema huishia kuharibika na kuhasiri wanaokila, ukawa msiba juu ya mwingine.

Ni muhimu kufahamu kuwa jukumu la kupambana na ukosefu wa chakula ni la kila raia. Hali ya kungojea kila mara kulishwa na serikali inatufanya kuwa wategemezi zaidi. Wakulima wadowadogo ambao huuza vyakula vyao kwa bei ya chini sana mara tu wanapovitoa mashambani wanapaswa kijiasa dhidi ya mazoea haya na kujua kuwa akiba haozi. Wanaoshi katika sehemu zenye vinamasi wasaidiwe kuzitunza sehemu hizi na kuzitumia kwa njia endelevu. Vijana wahimizwe wawaunge wazee mkono kushughulikia kilimo katika sehemu za mashambani badala




(a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 100 (alama 9,1 ya mtiriko)

Matayarisho




Jibu



GENIUS
EXAMS

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, eleza njia sita za kukabiliana na uhaba wa chakula.

FOR MARKING SCHEME CALL/WHATSAPP 0790906300



Jibu

GENIUS EXAMS



GENIUS EXAM 2024



3. MATUMIZI YA LUGHA

(alama 40)

- a) Eleza **tofauti** iliyopo kati ya sauti /e/na/u/

(alama 2)

- b) Onyesha **muundo wa silabi** ya kwanza katika maneno yafuatayo.

(alama 2)

(i) Ng'amua

(ii) Nchi

- c) Ainisha **vipashio vya kisarufi** katika sentensi ifuatavyo.

(alama 3)

Imeniwia.

- d) Geuza katika **hali yakinishi**.

(alama 2)

Hatutapita tusipoandaliwa vizuri.

- e) Andika katika **usemi halisi**.

(alama 3)



GENIUS EXAM 2024



Ojay alishangaa na kusema kuwa hakuamini alipata sifa nyingi vile katika Lugha ya Kiswahili.

.....

.....

.....

.....

- f) Onyesha **kijalizo** katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Yeye ni mwizi sugu sana.

.....

- g) Ainisha **vitenzi** vilivyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Juma angali barabarani na angali anaendesha baiskeli ambayo imechakaa.

.....

.....

.....

.....

GENIUS
EXAMS

- h) Ainisha matumizi ya kiambishi “**na**” katika sentensi hii. (alama 2)

Nina na Tina wanasaidiana na Dina.



GENIUS EXAM 2024



.....

.....

.....

.....

- i) Eleza **maana nne** zinazojitokeza katika sentensi hii (alama 2)

Alinipigia simu.

.....

.....

.....

.....

.....

- j) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha **vitenzi** kuwa **nomino**. (alama 1)

Mgeni alipofika wenyeji walifurahi

.....

.....

- k) Tunga sentensi moja kudhihirisha **wakati uliopita hali ya kuendelea**. (alama1)

.....

.....

- l) Bainisha **kirai vumishi** na **kirai elezi** katika sentensi hii. (alama 2)

Mwanafunzi mwerevu mno atatuzwa Disemba

.....

.....



GENIUS EXAM 2024



m) Kifo ni kwa mauko,..... ni kwa moyo na..... ... ni kwa ngeu. (alama 2)

n) Andika katika **udogo**. (alama 2)

Ukuta huo umejengwa karibu na barabara.

.....

.....

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia **kielelezo cha matawi**. (alama 4)

Yule jambazi aliyefungwa jela ni sugu.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

p) **Ainisha shamirisho** katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Kwa baiskeli, mzigo mzito wa mjomba Ali ulibebwa na Juma.

.....

.....

.....

q) Tunga sentensi mbili kubaini matumizi **mawili tofauti ya kibainishi**. (alama 2)



GENIUS EXAM 2024



.....

.....

r) Unda nomino **mbili mbili** kutokana na vitenzi vifuatavyo: (alama 2)

i. Jaribu

.....

.....

ii. Chuma

.....

.....

s) Bainisha matumizi ya '**kwa**' katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

i. Ameenda kwa Abadalla.

.....

.....

ii. Alipata alama sabini kwa mia.

.....

.....

GENIUS
EXAMS



Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Rais adinda kuweka kidole

Kinyume na matarajio ya wengi , rais jana aliwarejeshea wabunge mswada wa *'Finance Bill 2024'* ili waupige msasa. Inakisiwa kuwa huenda rais alifanya hivyo ili kutuliza ghadhabu za vijana almarufu *Gen Z...*

- a) Kwa kutolea mfano, tambua sajili hii. (alama 2)



- b) Thibitisha sifa nyingine **nane** ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)



GENIUS
EXAMS



GENIUS EXAM 2024



.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO



**GENIUS
EXAMS**